Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Wala msifanye uharibifu katika nchi ikiisha tulia. Na Mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Bila shaka Rehema za Allah zi karibu na wafanyao hisani. (Al-A'raaf 7:57)

JUZU 80 No. 215 | RAMAD.-SHAW.1440 AH | JUNI 2020 | IHSAN 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Dini ya Islam na Demokrasia kwa Waumini

Na Majlis Ansar Sultanul Qalam



HakikaAllahAnawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa adili; bila shaka mauidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana; Hakika Allah ndiye Asikiaye, Aonaye. [Surat An-Nisa' 59]

Amana - Yaani kazi au kitu ambacho mtu amekabidhiwa; au amri ya Mungu anayowapa watumishi Wake; au ahali za mtu. Mtume[saw]. alisema ya kuwa ***cheo au kazi yenye mamlaka pia ni amana*** (Muslim sura Imaarat)

Demokrasia ni mfumo wa nchi ambapo mamlaka ya kuongoza na au kuendesha nchi yanatokana na wananchi. Hufanyika kwa mfumo wa uwakilishi, ambapo mtu au kundi la watu huchaguliwa kila baada ya Muda maalum kuwakilisha Wananchi wengine. Mataifa yamekuwa na aina zao mbalimbali za demokrasia na uchaguzi. Kuna nchi zinaongozwa kwa mfumo wa Dini moja kama Saudia Arabia, Pakistani, Iran, Vatican Roma, Italy n.k na nchi zilizo nyingi zina Demokrasia ya mtu yeyote raia wa Dini yeyote anaweza Kuchagua na Kuchaguliwa kwa nafasi yeyote.

Dhana hii ya nchi za Demokrasia ya mtu yeyote wa Dini yeyote maadamu ni raia wa nchi husika kushiriki katika Uchaguzi imepingwa sana na baadhi ya makundi ya Kiislam hasa yenye mtazamo kuwa ni Islam pekee ndio inafaa Kuongoza hata kwenye nchi hizo. Yaani wasimike Dola ya Kiislam. Dhana hiyo ikajengeka kuwa ni Haramu kwa Muislam kushiriki kwenye Demokrasia ya Uchaguzi kwenye nchi hizo. Ingawaje lengo la Islam sio Dola. Maana Ustawi wa Islam hautegemei Dola. Nguzo za Islam sio dola na Nguzo za Islam zinatekelezeka hata bila kuwa na Dola. Katika nchi ambazo wote au asilimia kubwa ni Waislamu wanaweza kuanzisha Dola ya Kiislam kuongoza watu na sio kwa ajili ya Uislamu. Malengo ya Dini yapo mengi na kwa namna yake hutimizwa na hakuna lengo popote la Dola la Islam na wala Mtume[saw] hakufundisha hivyo licha ya kuwa Mfalme Nabii na Makhalifa wake. Sunnah hii ilitokea tu kama kwa manabii waliotangulia kuwa na dola na sio kwa manabii wote na hivyo sio Sunnah ya lazima kwa kuwa malengo ya Islam yanaweza kutimizwa hata bila kuwa na Dola.

Kila Dini inamalengo yake, Na malengo haya ya Dini takribani dini zote zina malengo yake matatu makubwa na Dini ya Islam pia ina malengo yake.

Endelea uk. 5

Chunga Matumizi ya Lugha; Hasa Mitandaoni!



Na Mtandao

Najua mnajua ila si vibaya tukakumbushana jambo hili ili kuimarisha matumizi yetu ya lugha katika jamii.

Katika jamii yoyote ile kuna mambo matatu huzingatiwa katika mawasiliano yao kulingana na tamaduni, desturi na kaida inayowaongoza ili kuifanya

Endelea uk. 4

UONGO

Hauna Nafasi Katu katika Islam

Na Mwandishi Wetu

Islam imeuweka uongo katika daraja la kwanza la uovu na pia ni shirk.

Yaani unategemea uongo kukusaidia kupatanisha au kujiokoa badala ya Allah. Hiyo ni shirk.

Hadithi unazozinukuu ama hujazielewa au vinginevyo, lakini Quran Tukufu inabakia kuwa hakimu kwa Hadithi na inatuonya: *"Na msiseme, kwa sababu ya uongo usemao ndimi zenu, hii ni halalu na hii ni haramu, msije mkamzulia uongo Allah. Hakika wale wamzuliao uongo Allah hawatafaulu."* 16:117

Kilichoruhusiwa katika Islam ni kufanya hila, na hizi Allah Naye huzitumia sana na anajisemea kuwa *"na wakafanya hila; na pia Allah Akafanya hila, na Allah ni MBORA wa wafanyao hila"* 8:31

Ona pale Mtume[saw] alipokuwa na Seyidna Abubakar[ra] wakikimbilia Madina, aliwauliza mtu kwamba je mumemuona Muhammad? Akajibiwa hapana. Hapa si kwamba alikana jina lake au alisema uongo bali alifanya hila hii ya kwamba Muhammad wako wengi, ila kama ingeulizwa Mtume Muhammad asingejibu namna ile.

Endelea uk. 4

Muongozo kwa Waqifeen-e-Nau uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kwa Heri Ndugu Benjamin William Mkapa

Mwanahistoria makini atakapokuwa anachunguza mchango wa historia ya Tanzania hatakosa kuona nyayo zilizo bayana za Benjamin William Mkapa – mwandishi mwenye hisia kali, muumini wa kweli na uwezo na aliyejenga falsafa ya kisiasa kwenye imani kuwa mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe.

Nyayo hizo zinazojitokeza kwenye mchango huu ni utumiaji wa vipaji, utamaduni wa kusoma, kuhifadhi historia, kutojitutuma, ujengaji hoja na kukubali makosa.

Benjamin William Mkapa, Rais wa awamu ya tatu wa Tanzania alitumia vizuri na kwa faida ya taifa lake na Afrika kwa ujumla umahiri wake wa kuandika ulisaidia katika kuamsha hasira ya kuchukia kutawaliwa na hivyo kuamsha jazba ya kutaka kujikomboa. Kalamu yake ilifanya kazi nzuri wakati akiwa mhariri wa gazeti la Tanganyika African National Union (TANU) ***Nationalist***. Tahariri ambazo aliziandika mwenyewe ni ushahidi ni kwa jinsi gani kalamu inaweza kutumika katika ukombozi. Mashairi yake katika lugha ya Kiingereza na makala alizoandika katika gazeti la Transition zote hizi zinatukumbusha nguvu ya kalamu kama walivyotumia Augustino Neto wa Angola, Leopold Sedai Seghor wa Senegal na Dennis Brutus wa Afrika ya Kusini. Kipaji pia cha kujieleza katika Kiingereza kiliweza kufikisha kwa usahihi madai ya wale waliokuwa wananyanyaswa na kuonewa na makaburu Wareno na walowezi kupitia Radio Tanzania wakati huo ikiiitwa External Service. Utumiaji wa kipaji ulichopewa na Allah kwa manufaa ya wengine ni neema kubwa iliyoambatana na baraka. Lipo tunaloweza kujifunza hapo; Tumia kipaji kuwatumikia binadamu.

Kuwatumikia binadamu ni jambo la faida kubwa ila halipatikani bila ya kuitafuta elimu kwa njia ya kusikiliza maoni ya wananchi na kusoma. Toka mwanafunzi, Benjamin William Mkapa alijenga mahaba makubwa ya kusoma. Ukipitia kitabu chake *My Life My Purpose*, anaeleza waandishi aliowahusudu akina Agatha Christie, Charlotte Bronie, Thomas Hardy, Chinua Achebe, washairi Alfred Tennyson, Lord Bryon, Shakesphere.

Katika udhaifu mkubwa tulio nao ni kupuuza umuhimu wa kusoma. Benjamin William Mkapa ametuachia somo kubwa katika kupenda kusoma.

Maendeleo ya kweli yanapatikana katika kufika ulipotoka na mnapoelekea. Historia ni chombo muhimu katika kuhifadhi mkusanyiko wa utamaduni, elimu, falsafa na mikakati yetu ya kwenda mbele. Historia inatusaidia matatizo na mafanikio ya waliotangulia ili tuweze kujisahihisha na kuyachukua yale yanayofaa. Kazi nzuri aliyoifanya Benjamin William Mkapa katika kuandika kitabu chake *My Life My Purpose* ni kazi inayotakiwa kuigwa na wananchi wa Afrika. Mambo yetu mengi yamepotea kwa sababu ya kutoandika mambo yetu ya utamaduni, Mila, dawa zetu, yote hayo yanapotea kwa sababu hatujaandika. Wapo Watanzania waliotufanyia kazi nzuri ya kuhifadhi historia yetu, Shaaban Robert – *Maisha Yangu Baada ya Miaka ya Hamsini*, Matias Mnyampala – *Historia ya Wagogo*, Erasto Mangenya – *Discipline and Tears*, Sophia Mustafa – *The Tanganyika, Life and Times of AbdulWahid Sykes*, Al-Noor Kassam, Edwin Mtei.

Tunatoa mwito kwa viongozi wetu watuachie hazina kama aliyotuachia Benjamin William Mkapa.

Viongozi wa Afrika wana sifa ya mbwembwe na kuwakoga wengine. Vyeo vyote ni mali yao, Mwenyekiti, Mkombozi, Jemedari. Na wakipitia wengine wote lazima wasimame Benjamin William Mkapa hakuwa na hulka ya kujikweza. Alipoingia madarakani akikataa kata kata kuitwa Mtukufu na alikataa picha yake kuwekwa kwenye fedha. Viongozi ni watumishi. Na mtumishi hawezi kuwa bora kuliko aliyemuajiri katika ule mkataba yaani katiba kila mtu amepewa wajibu wake. Katika hili amewaachia mfano mzuri kwa viongozi wale ambao kukumbwa na maradhi ya kulewa madaraka.

Kipaji cha kusikiliza maoni ya wengine, ukaheshimu kutofautiana kwetu lakini ukatoa uhuru wa mtu kujenga hoja hata kama hukubaliani naye ni alama ya kukomaa na kuheshimu mawazo ya mwingine. Lakini la muhimu zaidi ni umahiri wa kujenga hoja na kuthibitisha kwa mfano na takwimu hoja hiyo. Wakati wa Mkapa maua yalichanua ya rangi tofauti na alihimiza watu kutoa maoni yao kwani hakuna mwenye hati miliki ya mawazo yaliyo bora. Utamaduni huu ni jiwe kuu la pembeni la demokrasia. Waliokuwa hawamfahamu walimfahamu katika ule mhadhara akijenga hoja zilizowapika wagombea wenzake wa kiti cha Uraisi. Hahamaki, ghadhabu, jazba havisaidii sana kujenga nchi. Kubaliana kutofautiana na mshindi mwenzio kwa hoja iliyo bora zaidi. Somo kubwa kutoka kwa Benjamin William Mkapa; toa njia mbadala, umeonyesha kwamba nyumba imeanguka tuonyeshe namna ya kuijenga na kwa ajili ya maendeleo yetu 'Jenga hoja usipayuke'.

Kutambua utu wako, kuelewa kuwa binadamu ni dhaifu tena dhaifu sana na aliyekamilika ni Allah ni njia ya kufungua milango ya ushirikiano na kusaidiana kwani unatambua hukukamilika na hivyo unahitaji msaada. Kwa sababu ya kujua udhaifu wako kila unapokosea unaomba radhi. Ni dalili kubwa ya kutambua kuwa binadamu tunajifunza kwa makosa na kila tunapokosea tuombe radhi. Ni viongozi wachache katika bara la Afrika wanaoweza kuogelea katika maji hayo. Benjamin William Mkapa aliweza na manufaa ya Afrika tunawaombea nanyi viongozi wa Afrika muweze. Mungu Ibariki Afrika.

Tuhuma kwa Waislam Kumiliki Majini na Mapepo

Na Idara ya Tarbiyyat Taifa

Swali la muulizaji

Asalaam aleikum. Ndugu zangu wanajumuia kunaswali linanitatiza, kwa nini wengi sana Wakristu wanapenda kuituhumu dini yetu ya Islam kuwa tunamiliki majini, sijui mapepo? Naombeni majibu tuone tunahisi kwa nini wanawaza hivyoo au wanakua na picha hiyo.

Jibu kutoka Idara ya Tarbiyyat Taifa

Walaikum Msalaam Warahmatullah Wabarakatuh!

Sababu ni hii tu ya kwamba tangu kuzaliwa kwao Wakristo wamekuwa wakisikia kuwa Islam ni dini ya Majini na Mapepo kama wanavyosikia kuwa Islam ni Dini ya kigaidi na kuuwana (Jihadi).

Hivyo tangu makuzi yao wamekuwa wakipata taarifa za Islam ambazo si sahihi au zinazopinzana na Islam ya kweli tunayoiamini.

Katika hali kama hiyo hata kama waelezwe mafundisho sahihi ya Islam kwa hakika wanakuwa na changamoto kubwa sana kukubali mafundisho hayo ya kweli kwa sababu ya mafundisho ya uongo dhidi ya Islam yaliyokita mizizi katika mioyo yao tangu udogo wao mpaka sasa wamekuwa.

Hapa tunaweza kuona wasomi wa Kikristo wenye Shahada mbalimbali na hata maprofesa wakishindwa kung'amua na kukubali mafundisho ya kweli ya Islam, ambayo yamejaa hekima inayokubalika na akili ya kawaida kabisa ya Mwanadamu, yote hii ni kwa sababu tu iliyotajwa hapo juu.

Ukweli huu wapatikana pia kwa Waislam, kwamba kwa kuzaliwa tu ndani ya Islam, mtoto huwasikia wazazi na ndugu wa karibu wakinadi mara kwa mara kuwa Islam ndiyo Dini ya kweli, hivyo naye hukubali kuwa Islam ni Dini ya kweli naye huendelea kuwa Muislam tangu udogo wake mpaka anapokuwa.

Hakika ukitazama kwa kina ubora wa mafundisho ya Islam ambao uko bayana mno, utastaajabu ni kwa nini watu wanashindwa kuukubali ukweli huu, ila sababu ni hiyo tu iliyokwisha elezwa.

Hata kama watu hawa wataelezwa ukweli wa Majini na Mapepo, ugaidi na Jihadi kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Islam, ni wazi tu wataendelea kupinga kwa sababu hiyo.

Miaka ya hivi karibuni tumeshudia Khalifatul Masih V^{atba} akiwahutubia watu wa Mabara ya Ulaya na Marekani, na mara baada ya hotuba zake Wakristo wengi wanakiri kuwa hawakuwahi kusikia hapo kabla uzuri wa mafundisho ya Islam kama unavyoelezwa na Khalifa wa Ahmadiyya.

Hii inadhihirisha kuwa Wakristo wengi husikia mafundisho ya Islam kuwa ni ya ubaya kwa wanadamu kama vile kuogofya, Majini na mapepo, mauaji na ugaidi, chuki na visasi, ushirikina n.k jambo ambalo si la kweli lakini linaishi katika mioyo yao kwa muda mrefu kiasi cha kutoweza kukubali mafundisho mbadala wa imani na itikadi hiyo dhidi ya Islam.

Nini kifanyike katika hali hii?

Ili kuibatilisha imani yao hii dhidi ya Islam yatupasa kuendelea kwa kasi kueleza ubora na ukweli wa mafundisho sahihi ya Islam, kazi hii imefanywa kwa ustadi mkubwa na Masih Aliyeahidiwa^{as} na inaendelea kufanywa na MaKhalifa wake, nasi tufuate hatua hizi.

Tuishi kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Dini Tukufu ya Islam kama ilivyofundishwa na Allah na Mtume wake^{saw} na kuhuishwa na Masih wake^{as}, kwa namna hii tutayaweka wazi mafundisho sahihi ya Islam kwa majirani, wafanyakazi wenzetu na marafiki zetu, na sote kwa ujumla tutayaweka wazi mafundisho haya kwa jamii mzima inayotuzunguka.

Kwa muhtasari, namna bora ya kuishi kulingana na mafundisho ya Islam katika maisha yetu ya kawaida ni kutenda kila jambo letu kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Islam, Qur'an, Hadithi, Mafundisho ya Masih Aliyeahidiwa^{as} na MaKhalifa wake.

Kufanya kila kitendo chetu kwa ajili ya Allah na kutafuta radhi yake.

Tubadilishe vitendo vyetu tuvifanyavyo kama mila, tabia na mazoea na kufanya kwa kutafuta radhi ya Allah.

Kabla hatujafanya kitendo au jambo lolote, tufikiri jee? tunafanya kwa ajili ya Allah, kwa ajili ya Mtume wake^{saw}, Masih wake^{as} au Khalifa wake^{atba}?

Je? tunafanya kwa ajili ya kuitafuta radhi ya Allah?

Kama vitendo vyetu vyote vitakuwa na majibu ya ndiyo katika maswali haya, hapo tutabadili kabisa uelekeo wa maisha yetu na wa jamii inayotuzunguka na kwa pamoja tutalitimiza lengo la kuumbwa kwetu.

Islam imekuja kuondoa vitendo vya mila, tabia na mazoea vinavyofanywa na mwanadamu ambavyo kamwe mwanadamu hanufaiki navyo.

Badala yake vitendo vizuri vyote vitendwe kwa nia thabiti ya kuitafuta radhi ya Allah, hapo mwanadamu atapata malipo ya vitendo vyake toka kwa Allah sawa na Ahadi ya Allah na atakuwa na uhakika wa kuvidumisha katika maisha yake yote na hivyo kuendelea kupata malipo kutoka kwa Mola wake.

Ikumbukwe vitendo hupimwa kwa nia yake na mwisho wake sawa na hadithi za Mtume^{saw}.

Hivyo kama tunasali, tusisali kwa mazoea tu, kwa sababu baba anasali nami nasali au kwa sababu nipo hapa Masjid na wakati wa Sala umefika basi nasali la, tuwe na nia thabiti kwamba ninasali kutekeleza amri ya Mola wangu na kuitafuta radhi yake.

Vivyo hivyo kwa vitendo vyetu vingine kama kula, kulala, kutembea, kufunga, kuhiji, kusoma, kujitolea mali, wakati na heshima, kutafuta riziki, kufanya kazi n.k.

Kwa kufanya hivyo si tu kutaibadilisha hali ya Wakristo waliyonayo sasa bali itatubadilisha nasi na kutupandisha Madaraja ya kiroho na kutufanya tuishi pamoja na Manabii, Masiddiki, Mashahidi na Masalih.

Tunamuomba Allah Atujaalie sote kuishi sawa na matarajio ya Masih Aliyeahidiwa^{as} na Khalifa wake^{atba}. Amin

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ufahamu Muongozo kwa Waqifiin-e-Nau

Imefasiriwa na: **Ahmad Abdul Nasibu**



Khalifa Mtukufu wa V^atba akihutubia Ijtimaa ya mwaka ya Waqf-e-Nau Uingereza mwaka 2015

Mpango wa Waqf-e-Nau ulianzishwa na Hadhrat Khalifatul Masih IV (rh) mnamo tarehe 3 Aprili 1987. Maana ya neno Waqf ni kujitoa kwa kusudi jema na madhumuni ya mpango wa Waqf-e-Nau ni kwa wazazi kuwatoa watoto wao kwa ajili ya kuizagaza Islam kabla ya kuzaliwa kwao. Baada ya mtoto kuzaliwa, wajibu wa wazazi hauishii hapo bali wanapaswa kuhakikisha makuzi ya mtoto wao yanafanyika katika namna iliyo bora. Wanapaswa kujiambatisha kwa Khalifa wa zama na kupaswa kutambua kuwa wana wajibu mbele ya Jamaat. Orodha ya miongozo inawasilishwa mahsusi kwa Waqifiin-e-Nau kutoka kwenye hotuba zilizotolewa na Mtukufu Hadhrat Khalifatul Masih V atba.:

Elewa Umuhimu wa Kiapo chako:

"Unapaswa kukumbuka daima kwamba wewe ni sehemu ya Jamaat ambaye wazazi wake wameweka ahadi na Allah kutoa maisha yako kwa ajili ya Jamaat na Islam. Kwa hiyo, elewa daima na tambua umuhimu wako, na katu usivunje ahadi ambayo wazazi wako wamefanya. Kwa maneno mengine, wazazi wako wamefuata mfano wa Hannah, mama wa Hadhrat Mariam. Dhabihu ya kweli aliyotoa na mfano aliouonyesha umetajwa katika Sura Al-Imran, ambapo inasema: '(Kumbukeni) aliposema mwanamke wa Imrani: Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye. (Sura 3, aya: 36) Wengi wenu aidha mna miaka 15 au zaidi na mmechagua kuhuisha kiapo hiki cha kujitoa kwa huduma za Jamaat. Ili kutimiza kiapo ambacho awali kiliwekwa na wazazi wako, wapaswa kujiwasilisha rasmi kwa Jamaat na kutoa huduma zako, punde unapomaliza elimu yako. Tayari, kuna kundi miongoni mwenu ambalo limejiunga Jamia Ahmadiyya na kuweka kiapo kuihudumu Islam, hivi sasa linajiandaa kwa ajili ya kazi kubwa mbeleni. InshaAllah, mwaka huu, kundi la kwanza la wabashiri litahitimu kutoka Jamia Uingereza na litaweza kutimiza kiapo kilichowekwa awali na wazazi wao na baafaye kuhuishwa na wenyewe kwa nafsi zao. Allah Awajaalie wote uwezo wa kufanya hivyo. Hata hivyo, mbali na wale wasomao Jamia, kuna Waqf-e-Nau wengine wengi ambao wanayaendea maeneo ya masomo. Mnapaswa kukumbuka daima kwamba unaweza kujihesabu kiukweli kama Waqf, kama baada ya kumaliza masomo yako, ukajiwasilisha kwenye Jamaat." (Hazrat Khalifatul Masih V^atba – Ijtima ya Taifa ya Waqf-e-Nau, UK 6 May 2012,, Baitul Futuh, London)

Kutimiza Majukumu yako ya kidini

"Kuichunga sala yako kwapaswa kuwa chapa ya Waqf-e-Nau, na hili linahitaji mara zote uchunge sala tano za faradhi na kuzisali kwa adabu kamili na umakini. Pia uzingatie kusali sala za nafal kadiri iwezekanavyo. Uisome Qur'an Tukufu kila siku na kujifunza tafsiri yake na maana zake za kina. Haitoshi tu kusoma Qur'an Tukufu; unalazimikia pia kufanya kwa vitendo kile Qur'an inachokufundisha. Masuala yote haya ni ya msingi kwa kila Waqf-e-Nau. Unapoyafanya na kutimiliza mahitaji haya ya msingi, ambayo ni lazima kwa ukuaji wako mzuri wa kimaadili, hapo tu ndipo utaonekana kama mtu ambaye kila tendo lake ni kwa ajili ya kupata ridhaa ya Mungu. Ndipo utakuwa mtu ambaye anatengeneza maunganiko ya kweli na Allah na utakuwa yule ambaye kiukweli anahangaikia kupata mapenzi Yake."

(Hazrat Khalifatul Masih V^atba – Ijtima ya Taifa ya Waqf-e-Nau, UK 6 May 2012,, Baitul Futuh, London)

Waqf-e-Nau anatakiwa kutoa kipaumbele kwenye majukumu ya dini juu ya masuala ya kidunia

Kumbukeni aliposema mwanamke wa Imrani: Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye. (Sura 3, Aya 36)

Akiifafanua aya Mtukufu Hadhrat Khalifatul Masih V (Atba) alisema: "Kama nilivyosema, Nimelielezea hili kwa kina mara nyingi hapo kabla. Hakuna mtoto wa Waqf-e-Nau apaswaye kufikiria kwamba kama wakijitoa Waqf namna gani watajipatia mahitaji ya maisha, wala wasiwazue wazo la namna gani watawasaidia wazazi wao kifedha au kimwili. Hivi karibuni, niliongoza darasa la Waqf-e-Nau hapa [Toronto] ambapo mvulana aliuliza kwamba endapo baada ya Waqf tunajitoa kiukamilifu kwa Jamaat, basi namna gani tutaweza kuwatunza wazazi wetu kiuchumi, kimwili, au matunzo ya kiujumla? Uibukaji wa swali hili inaashiria kwamba, tangu utotoni, wazazi hawakulisanikisha kwa mtoto wao wa Waqf-e-Nau utambuzi kwamba tumekutoa na sasa uko na sisi tu kama watunza amana wa Jamaat. Ndugu zako watatutunza; wewe unatakiwa tu kujiwasilisha mbele ya Khalifah wa zama na kufanya sawa na maelekezo yake."

"Neno hasa: حُرّ lililotumika katika dua ya mama yake Hadhrat Mariam^as linamaanisha kwamba nimejitenganisha kiukamilifu na mwanangu huyu kutoka masuala ya kidunia na ni maombi ya yangu ya dhati kwamba kipaumbele chao pekee kiwe kutekeleza majukumu ya dini."

"Tokea utotoni, Waqifeen wanapaswa kufundishwa kwamba hakuna kitu cha maana kuliko Waqf-e-Zindagi [kujitoa maisha]. Badala ya kuangalia katika mafanikio ya kidunia ya wengine, au ya mwanafunzi mwenzangu, baada ya kupata elimu inayoshabihiana, anapata mamia ya maelfu [ya dola] wakati mie sipati kwa mwezi wanachokipata kwa siku, fikira zao ziwe kwamba heshima Aliyonipa Allah ni kubwa kuliko mafanikio ya kidunia. Watu wanapaswa kujikumbusha mafundisho ya Mtukufu Mtume Muhammad saw ya kuwaangalia wale wenye bahati kidogo kuliko wewe kuhusiana na utajiri wa kimwili na kuwaangalia wale walio na bahati zaidi yako katika masuala ya kiroho. Kwa hiyo, hususan wavulana Waqf-e-Nau ambao wamemaliza elimu yao, wanapaswa badala ya kuboresha hali zao za kidunia, wafanye juhudi kupiga hatua katika uchamungu. Masihi Aliyeahidiwa as alitegemea kila Muislam Muahmadiyya kuwa na viwango vya juu sana, sasa fikiria kiasi gani juhudi zinatakiwa kufanywa na watu ambao wazazi wao wamewatoa kwa ajili ya imani kabla ya kuzaliwa kwao na wakawaombea."

(Hadhrat Khalifatul Masih V^atba – Hotuba ya Ijumaa – 28 Oktoba 2016)

Waqf-e-Nau wanapaswa pia kutoa muda katika mipango mingine ya tanzim

"Kwa ufupi, ningependa kuweka msisitizo katika baadhi ya taratibu na masula ya kiuongozi ya Waqifeen. Baadhi ya watu wameibua hili suala kwamba baadhi ya Waqifeen-e-Nau wana dhana potofu katika akili zao kwamba, baada ya kuwa mwanachama wa Waqf-e-Nau, wamepata utambulisho mbali mbali. Wanao utambulisho bainishi, lakini hili haliwapi wao upendeleo wowote wa ziada. Badala yake, pamwe na utambulisho huu, wanategemewa kuongeza hali zao za kujitolea. Baadhi ya watu wanapandikiza mawazo kwa watoto Waqifeen-e-Nau kwamba wao ni watoto maalum sana, ikasababisha wao

Endelea uk. 4

Ufahamu Muongozo kwa Waqifiin-e-Nau

Kutoka uk. 3

wajihisi ni maalum wanapokuwa watu wazima. Na hapa pia, nimehabarishwa juu ya matukio ambapo watu wa namna hii kutojali uhalisia wa Waqf hapo hapo wakifanya lengo la maisha yao kuwa na jina tu la Waqf-e-Nau, wakiamini litawafanya kuwa maalum. Wengine wanaamini kuwa kwa sababu wao ni Waqf-e-Nau, wamesamehewa kuhudhuria mipango ya tanzim zao – iwapo ni wasichana, zile za Nasirat au Lajna, au kama ni wavulana, zile za Atfal au Khuddam; kama vile kusema, "Tanzim yetu ni tanzim mbali mbali kabisa." Kama wazo hili lipo katika moyo wa yeyote, ni potofu kiukamilifu. Afisa yeyote wa Jamaat, hata awe ni Amir Jamaat, ni mwanachama wa tanzim muambatano na umri wake. Hivyo, kila Waqf-e-Nau msichana na mvulana mnalazimika kukumbuka kwamba ni wanachama wa tanzim inayolingana na umri wake – vyovyote umri wake utakavyokuwa, wanatakiwa kushiriki katika programu zao. Na kwa wale wasioshiriki, kiongozi wa tanzim husika anapaswa atoe ripoti. Na kama hili halimrekebishi [mtoto], basi mtoto kama huyo atatolewa kutoka mpango wa Waqf-e-Nau."

(Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} – Hotuba ya Ijumaa – 28 Oktoba 2016)

Kada gani Waqf-e-Nau anapaswa kuiandama?

"Kama nilivyosema, katika hatua mbalimbali za masomo yenu, muiulize Jamaat kada ipi ya kuiandama-badala ya kuchagua kada wenyewe.

Kuhusiana na uchaguzi wa shughuli, pia nimesema hapo kabla kwamba Waqifeen-e-Nau wavulana watoe upendeleo wa kwanza katika kuingia Jamia na kuwa wabashiri; hivi sasa kuna hitaji kwa hili. Kutokana na fadhila za Allah Mwenye nguvu, Jamaat inapanuka. Sio tu Jamaat mpya zinaanzishwa katika maeneo ambapo Jamaat ilishaanzisha kitambo, bali Allah Mtukuka pia Anatupatia Jamaat katika nchi mpya. Na tunahitaji wabashiri chungu nzima katika kila nchi. Kisha, hospitali zetu zinahitajia madaktari. Huko Rabwah, kuna hitaji kubwa la madaktari na mabingwa mbalimbali. Huko Qadian, hospitali ipo na haja ya madaktari. Kama kuna madaktari wasio Waqf wanaosikiliza hotuba yangu ambao hawawezi kupelekwa katika sehemu hizi, basi wawaekee msisitizo watoto Waqf-e-Nau katika nchi zao kuelekea kuwa mabingwa. Kuna uhaba wa madaktari bingwa. Pia kuna haja ya madaktari wa kila nyanja Afrika. Halafu, huko Guatemala, hospitali kubwa inajengwa ambayo inaweza kutembelewa kutoka Canada. Hapa, kuna haja ya madaktari ambayo itaongezeka hapo baadaye. Kuna haja huko Indonesia (kwa ajili ya madaktari), na haja itaongezeka popote Jamaat itakapotanuka. Kwa hiyo, watoto wa Waqf-e-Nau ambao wanapenda kuwa madaktari, baada ya kupata elimu ya juu na kubobea, wajitokeze mbele na kwenda katika nchi ile ambayo ni rahisi kuitembelea. Jiwasilisheni, kisha Jamaat itawatuma. Vivyo hivyo, shule zina hitaji la walimu. Wasichana na wavulana wote wanaweza kutumika kama madaktari na walimu, kwa hiyo lipeni hili umakini wenu. Pia kuna haja ya wachora michoro na wahandisi ambao ni wataalamu katika kujenga majengo ili kwamba upangaji mzuri na usimamizi vinaweza kukidhiwa katika ujenzi wa misikiti, nyumba za wabashiri, shule, hospitali, n.k., ambao utaokoa fedha za Jamaat; nyenzo bora zitaweza kujengwa kwa gharama ndogo. Pia kuna haja ya wahudumu wasaidiao madaktari, hivyo [Waqifeen] waingie katika kada hii pia. Hivyo, hizi ni baadhi ya kada maarufu kuhusiana nazo Jamaat hivi sasa inahitajia. Hapa baadaye, mahitaji yatabadilika sawa na hali ya mambo".

(Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} – Hotuba ya Ijumaa – 28 Oktoba 2016)

Tunahitaji Waqifeen katika tafiti za kisayansi

Baadhi ya Waqf-e-Nau wana shauku katika kada fulani mahsusi, na pindi wanaponiuliza, nikizingatia shauku zao, ninawaruhusu kusoma [katika kada ile mahsusi]. Lakini hapa nataka kuwaarifu wanafunzi kwamba wazifukuzie kada mbalimbali za tafiti za kisayansi- na hii inawajumuisha Waqifeen-e-Nau na wanafunzi wengine. Kama tukizalisha wanasayansi bora katika kada mbalimbali za tafiti za kisayansi, basi hapo baadaye Waislam Waahmadiyya watakuwa ndio wenye kutoa elimu ya dini. Na ambapo dunia itakapokuwa na haja na elimu yenu ya dini, watakuwa pia na haja nanyi kwa ajili ya elimu ya kidunia. Katika muktadha huu, Waqifeen-e-Nau watakuwa na kazi za kidunia, lakini lengo la kazi yao na elimu litakuwa kudhihirisha Umoja wa Allah Mwenye nguvu na kusambazaji wa dini Yake.

(Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} – Hotuba ya Ijumaa – 28 Oktoba 2016

Uongo Hauna Nafasi Katu katika Islam

Kutoka uk. 1

Jibu kama hili alikuwa akiwapa pia Masahaba walipoomba ushauri binafsi, nao walimuuliza *unasema kama Mtume au Muhammad*? Na alijibu "*nakushauri kama Muhammad*".

Uongo hauna nafasi katu katika Islam, tusiuhalalishe kwa tamaa za nafsi zetu!!!

Majibu hayo ni mazuri na ni sahihi.

Pia unaweza kuongeza kwamba kinachokusudiwa katika hadithi hizo ni kwamba katika kupatanisha mke na mume au baina ya makundi mawili na hata katika vita sio lazima useme ukweli wote unaoujua (mithili ya walle Wakristo wanaoungama). Bali unachotakiwa ni kueleza jambo lile tu ambalo halitochochea zaidi ugomvi na kuzuia mapatano au kama ni katika vita halitompatia adui taarifa za kukushambulieni.

Na ieleweke kwamba kutokueleza ukweli wote unaoujua sio kusema uongo.

Kwa mfano kama mtu unapatanisha baina ya mke na mume na unavijua vitendo vichafu vya mmoja wapo, sasa iwapo utavieleza hivyo ukidhani kwamba ndio mwingine ataridhika bila shaka utakuwa unaongeza chumvi kwenye kidonda, bali lililo sawa ni kujaribu kuzinyamazia aibu unazozijua na kumsihi mwingine asamehe yaliyopita na kuishi na mwenzake kwani katika hilo zipo faida ndani yake.

Mifano ya aina hii iko mingi, lakini sio kusema **uongo**. Uongo ni katika madhambi makubwa yanayoangamiza na haiwezekani Uislamu ambao unajitaja kuwa ni dini ya hekima hairuhusu kufanya dhambi kwa kisingizio cha kuondoa tatizo fulani.

Chunga Matumizi ya Lugha!

Kutoka uk. 1

jamii hiyo ielewane kwa urahisi bila kukwazana. Mambo hayo ni muhimu yanayoifanya jamii ielewane kwa urahisi na kuheshimana kupitia lugha yanazingatia kwa kutegemea na yafuatayo:

1. Mada

Namna ya uchaguaji wa maneno ya kutumika yanahusiano mkubwa na mada inayojadiliwa, hii ndio kusema maneno fulani au utamkaji fulani unaweza kuwa sahihi katika mada moja na asije sahihi katika mada nyingine. Mfano kama mada inahusu uzazi, agharabu unaweza sikia via vya uzazi vikitajwa na kusiwe na tatizo wala ukakasi masikioni kwa wasilikizaji au wasomaji wa hiyo mada lakini katika mada nyingine ikaleta ukakasi katika masikio kuvitaja hivyo via vya uzazi hadharani.

2. Uhusiano Wa Wazungumzaji

Hili nalo ni muhimu kulifahamu na kulizingatia wakati wa kuchagua maneno ya kutumika katika mazungumzo kwasababu neno moja laweza kuwa sahihi kwa mtu mmoja lakini lisiwe sahihi kwa mtu mwingine. Kwa mfano huwezi muita baba yako "Oyaa" lakini unaweza kumuita wa rika moja na wewe kulingana na mada mnayozungumza na mahali mlipo. Katika siku za karibuni vijana wengi wameshindwa kuzingatia hilo na kujikuta wakitumia maneno yasio sahihi kwa watu bila kuzingatia uhusiano walio nao na hatimae kujikuta wakihesabika kuwa hawana nidhamu na wasio na adabu kumbe alikuwa na nia njema lakini tatizo lililopo ni kushindwa kuchagua neno sahihi la kulitumia wakati huo

3. Mahali

Mazingira yetu yana desturi na heshima tofaut vivyo hivyo ni muhimu kuchagua maneno ya kutumia kulingana na asili na hadhi ya eneo husika kwasababu neno ambalo linatumika bandarini kwa wabebaji mizigo katika kuhamasishana kazi haliwezi kutumika msikitini au ofisin na ukilitumia utahesabika kuwa umetukana na huna adabu ilihali Bandarini ni neno la kawaida linalotumika na mtu mwenye heshima zake na wote wanaolisikia hawapati ukakasi masikioni mwao. Hivyo muhimu katika maisha yetu ya kawaida tuwe tunatafakari maneno ya kuyatumia kabla hatujafumbua mdomo au kuandika ili kuepusha mgongano wa hisia hasa kwa kuzingatia nani unaezungumza nae, mnazungumzia nini na wapi.

Hitimisho

Katika makundi, wengi hatujuani ila uhusiano wetu ni wanajamaat hivyo tunakutanishwa na dini hivyo tunapojadiliana tujue kuwa tupo katika mazingira ya dini ambapo huwezi zungumza kwa kumkejeli mtu, kumkaripia au kumdhalilisha mtu kwani kifanya hivyo ni sawa na kumtusi jambo ambalo halikubaliki katika dini. Isitoshe kwa vile wengine hatujuani kwa sura huenda unaweza ukamjibu mtu mwenye umri wa baba yako kwa maneno yasiyostahili kumwambia baba yako hivyo ni vema tutumie maneno ya staha sawa na mazingira ya dini ambapo hakuna atakayekwazika imma mdogo au mkubwa.

Allah Atufanyie wepesi katika uchaguzi wa maneno sahihi ya kutumia katika mawasiliano yetu ili uwepo wa makundi uimarishe udugu wetu wa kiroho badala ya kututenganisha. Amin !

Dini ya Islam na Demokrasia kwa Waumini

Kutoka uk. 1

1. Kumjenga mwanadamu kuhusiana na Mungu wake,

2. Ibada, Kumfanya mwanadamu Kumuabudu Mungu Allah, na

3. Mwanadamu kutumikia wanadamu wenzake na viumbe wengine wa Allah.

Malengo mawili ya mwanzo ya Uhusiano wa mtu na Mungu na Ibada yanahusiana na Dini husika moja kwa moja pekee. Na lengo la tatu la kuhudumia watu na viumbe wengine huifanya Dini kuhusiana na Dini zingine na watu na viumbe wengine. Watu katika dini husika hushirikiana kutimiza lengo hili. Katika Jamii moja yenye itikadi tofauti za Dini hukaa pamoja na kuchagua yeyote kuongoza na kutimiza wajibu huu.

Mfano halisi wa kuhudumia viumbe na watu ulioelezwa ndani ya Quran Tukufu ni njia ya **Kujitolea** na katika Kujitolea kuna kujitolea Mali na Nafsi. Kujitolea Mali ilivyoelezwa ni katika njia ya kutoa sawa na Kipato chako, Zaka, Sadaka, Fidia n.k. Kujitolea Nafsi ni mtu mwenyewe Kujitoa kuwatumikia watu na viumbe wengine. Amri ya sala na zaka, kujitolea ni amri zilizoelezwa mara nyingi sana ndani ya Quran Tukufu na kwa pamoja, yaani **timiza ibada na uwahudumie viumbe.** Mifano kadhaa imeainisha ndani ya Quran Tukufu juu ya kujitolea, kujali Dini kwa Wazazi, Wasafiri, Masikini, Majirani, Wagonjwa, Wenye njaa na Kiu n.k. Hawa wote sio lazima wawe Waislam na sehemu kadhaa imeelezwa ndani ya Quran Tukufu kuwa msaada unaotolewa na asiye Muislam kwa Muislam mwenye dhiki au Jirani aupokee.

Allah amesema ndani ya Qur'an Tukufu Surah 5:21

Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: ***Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu, Alipowafanya Manabii kati yenu na Akawafanyeni wafalme,*** *na Akawapeni ambayo Hakuwapa wo wote ulimwenguni kote.*

Kwa namna hiyo Allah Akauugawanya Uongozi wa binadamu katika Makundi Mawili; **Unabii** na **Ufalme.**

Nabii ni mtu anayetumwa na Mungu kuja kuwaongoza wanadamu Kuungana - Kuhusiana na Allah na Kumhimidi Yeye pekee na huwafunza namna bora ya kuwahudumia viumbe. Mfalme hutokana na watu kwa njia yeyote iliyotumika na kukubalika kuwaongoza watu kwa lengo la kuwahudumia watu. Hutokea Manabii kuwa pia Wafalme kama Nabii Daudi[as], Nabii Suleiman[as], Nabii Yusuph[as], Muhammad[saw] n.k na sio kila Nabii ni Mfalme pia mfano Zakaria[as], Yahya[as], Isa bin Mariamu[as] (Yesu - Dini ya Ukristo inapatikana hapa)[as] na Ilyasa[as]

Baadhi ya Watawala waliingiwa na Hofu kwa wanadini kutawala ila mifano kadhaa iliyoonyeshwa kwa Manabii wote watawala ni wa kuigwa. Hawakuonyesha Ubaguzi wa Dini katika Utawala wao. Waliheshimu mawazo na rai za wengine hata kama sio wenye dini zao. Mtume[saw] mfano alipokuwa Mtawala alitoa Hukumu ya Kupigwa mawe mpakani kufa kwa mama Muyahudi alizinifu kwa



kwa kusikiliza rai ya hukumu ya makasisi wa Kiyahudi. Mtume[saw] alikopa kwa Myahudi mmoja deni. Waislamu mbalimbali Walikopa na kufanya kazi kwa watu hata sio Waislamu. Mifano hii michache inatuonesha jinsi Muislam anavyolazimika kuchangamana na jamii inayomzunguka na kuwa sehemu ya jamii hiyo kwa kila nukta. Pia katika haki hii ya yeyote kutumika katika Kuhudumia watu Nabii Yusufu[as] alichaguliwa Kutumika katika Ufalme usio kuwa na Dini yake. Surah.12:55

Na mfalme akasema: **Mleteni kwangu, nimchague kwa ajili yangu mwenyewe.** Basi alipozungumza naye, akasema: Hakika wewe leo kwetu u mwenye heshima, mwaminiwa.

Allah Alitaka Kutuonyesha kuwa ni yeyote anaweza Kuchaguliwa au kuchagua kwenye nchi yake. Na Nabii Yusufu[as] aliongoza kwa kutumia kanuni za Mfalme 12:77 kuwa sio lazima na Haramu Kuongoza kwa kutumia Sheria zisizo za Kiislam, maadamu nchi hizo zinaendelea kutoa Uhuru wa Kuabudu. Fursa zilizopo kwenye nchi mbalimbali za uchaguzi ni jukumu la kila mwenye sifa katika nchi husika kushiriki katika uchaguzi (kuchagua na kuchaguliwa). Ni wajibu wa lazima kwa Muislam kushiriki katika Uchaguzi kwa kuwa ni agizo la Allah kuwa katika **Uchaguzi mchague aliye mwadilifu - ADL 4:59** Waislamu wasipo shiriki wana dini wasipo shiriki ambapo Waislamu kadhaa wakiwa chama tawala na wengine upinzani. Hivyo chama chochote au kundi lisitumike kushawishi wengine wasishiriki kwenye siasa.

Lengo la wanadini kujihusisha na siasa ni kuchagiza umuhimu wa Uadilifu katika Demokrasia na Uaminifu. Na namna hii itaongeza msukumo wa kuwahudumia wananchi na viumbe vyote katika nchi hii. Wanadini wasiingie kwa lengo la kuwafanya wengine kuwa wanadini wao au kuitangaza Dini yao. Mtume[saw] hajawahi na hakutumia Utawala wake kunfanya mwingine awe Muislam na ndivyo kwa Nabii Yusufu[as] hata kwa Nabii Suleiman[as] Islam hairuhusu Shuruti katika Dini 2:257 hairuhusiwi kutumia njia ya kuwahudumia watu kama njia ya kuwashawishi watu wengine kuingia kwenye Dini. Waila mtu yeyote atakaye shawishika kuingia kwenye dini kwa wema aliotendewa hakatazwi kuingia kwenye dini. Katika janga hili la Korona, Khalifatul Masih V Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] aliziagiza Jamaat na watu wenye uwezo kuwasaidia watu bila kujali dini zao. Waahmadiyya katika nchi mbalimbali kama Uingereza, USA, Uganda, Canada, Ghana n.k waliwahudumia watu kwa chakula, vifaa na matibabu. Wapinzani wa Ahmadiyya wakapiga kelele kusema tunatumia njia hii kuihubiri Ahmadiyya. Khalifa wa Islam akajibu kuwa wanafanya hivyo kuwahudumia watu na sio sababu ya kuihubiri Ahmadiyya na Allah Anajua Nia zetu. Huko Canada inaelezwa kuwa mama mmoja pindi mtoto wake alipozidiwa usiku na huduma zote za misaada kushindikana aliombamsaadakwa taasisi ya vijana wa Ahmadiyya nchini Canada naye alisaidiwa kwa namna ya kipekee, lakini bado hakujiunga na Ahmadiyya na wala Ahmadiyya haikujutia msaada wake ila kumshukuru Allah kutimiza wajibu wake huu wa kuwahudumia viumbe wake.

Hivyo Wanasiasa wasioogope kwa Waislamu kuwa katika Siasa na Waislamu wasitumie Dini kama njia ya ushawishi kwenye siasa. Lengo ni kuwafanya watu wote kupata huduma sawa kwa Uadilifu bila kujali dini zao. Sifa moja ya Allah ni ya Rehema na Rehema zake imekienea kila kitu 7:157 na ndivyo kila mtu Rehema alizojaliwa na Allah zinapaswa kukienea kila kitu.

Islam inaruhusu Demokrasia kufanyika, Uchaguzi ufanyike 4:59, Viongozi watakao chaguliwa wawe Waadilifu 4:59, Wafanye mambo kwa majadiliano na Mashauriano 42:39. Hivyo Demokrasia ya Uongozi unaopata mamlaka kutoka kwa watu, dini imekwisha iruhusu na kuelezewa bayana namna ya utekelezaji wake kwa Manabii kadhaa, Kundi la Manabii kama Daudi, Suleimani, Ayubu, Yusuf, Musa na Harun, ambao ni Manabii waliopewa mamlaka, mali na ustawi, na hivyo wakaweza kuwatendea wema wanadamu. Hivyo Manabii wa kundi hili wameitwa **Al-Muhsiniin**, yaani, **wafanyao hisani**. Daudi na Suleimani walikuwa wafalme. Yusuf na Ayubu walipewa ustawi baada ya kujaribiwa kwa mateso na kuonyesha subira kubwa. Musa na Harun walikuwa na mamlaka makubwa kati ya watu wao.

Mwaka huu nchini Tanzania tunaingia kwenye uchaguzi. Waislamu na wasio kuwa waislamu wenye sifa za kuitumikia Taifa hili wanapaswa kushiriki kuchagua na kuchaguliwa. Uchaguzi hauwezi kufanyika ikiwa wananchi hawata shiriki kugombea kwenye nafasi za Udiwani, Ubunge, na Urais. Nafasi hizo zisipogombaniwa uchaguzi hautakuwepo na wakijitokeza kugombea na wasipopatikana kupiga kura haitakuwa na maana ya wagombea. Na huenda tukapata kiongozi mwema, hivyo tupige kura kuchagua kiongozi bora na wema kwa ustawi wa nchi yetu.

KUMRADHI

Makala ya "*Hizbu Tahriri Wakwama kwenye Vipimo*" Itaendela panapo majaaliwa toleo lingine.

Bustani ya Washairi

MAISHA

Mh! Najiuliza, maisha ni kitu gani
Kwani nikiyapuuza, kitanitokea nini
Na kama nikijikaza, nitayatoboa lini
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Tangu nilipozaliwa, kuja hapa duniani
Bado sijayaelewa, maisha hasa ni nini
Kwa kweli ningelijua, leo ningelishawini
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Magumu ninasikia, kwa wote ulimwenguni
Wale walotabikia, yamewakaba shingoni
Wengine nashuhudia, walalama midomoni
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Kisomo kunipatia, maarifa ya kichwani
Machombe na mama pia, kunipeleka shuleni
Wakidai ndio njia, kufaulu maishani
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Elimu niloipata, dah! Nipo hasarani
Mada nyingi nimekata, maana sijabaini
Maisha bado utata, ni kweli yapo shuleni?
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Jicho nikiliinua, kuona huko chuoni
Kucha nikisimamia, kufika huko kazini
Kicheko najichekea, maisha kweli utani
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Shauri nimelikata, kujitoa mashakani
Shairi naliambata, kupika kwa makuhani
Makungwi mkilipata, nijibuni naombeni
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Mbanga likishakufika, Mtwarako ndanindani
Usikose kuandika, mwana nitajua lini
Kikapu ninakutwika, ukitue kwa makini
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Wa Mamba sijakuvuka, naomba yako maoni
Unipe ninachotaka, usinitupe shimoni
Mjukuu kianguka, utamlaumu nani
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Wamwera babu wa kale, kijana nipo mbioni
Tumbua wangu upele, usumbuao kichwani
Tena piga makelele, waliyoshindwa shuleni
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Shunda Mshundia Wana, Mazongera nawe ndani
Abasi Mlea Wana, na Msomi makondeni
Ni wengi nilowaona, nielezeni jamani
Hakika nipo taabani, maisha ni kitu gani?

Zaid A. Machombe (mdogo)
Kitonga, Dar es salaam

SHANKUPE

1. Umefanyiwa huruma, hifadhi 'mepatikana
Unapaswa kujituma, ndoa tamu tena sana
Sipende kusemasema, unatukwaza vijana
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

2. Si kweli umbea sunna, haifai kina mama
Kupiga zogo hakuna, pika chakula mapema
Mkiacha kuzozana, dhambi hamtazichuma
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

3. Embu kaeni nyumbani, faida ni nyingi sana
Na msome Quruani, someni tena na tena
Msiseme ya chumbani, kwa mashoga watanena
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

4. Pia muwe na mipaka, kuchagua marafiki
Wanja mwingi 'takupaka, wengine ni mazandiki
Nanena kwa uhakika, bila shaka bila chuki
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

5. Shankupe jichunguze, mwendo wako si mzuri
Unafanya tukupuze, hata kama ni mzuri
Ndoa ngumu jilegeze, jifukizie uturi
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

6. Umetegesha sikio, dirishani kwa jirani
Kusikia ya wenzio, kuyamwaga koridoni
Kwa kweli tabia sio, ubadilike jamani
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

7. Kila mada waijua, unakalia kitako
Nyumba hii nawajua, wanashindia ukoko
Wakikosa vitumbua, shida nini fanya yako
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

8. Usichunguze ya watu, mjini patakushinda
Embu kwanza kua mtu, heshima itakulinda
Roho imejaa kutu, umbea unaupenda
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

9. Ndoa hii haidumu, mishipa 'mekusimama
Maisha ni gurudumu, linakwenda zima zima
Watu wakikutuhumu, utasutwa wewe mama
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

10. Mara maisha ya shida, ndo mana wanapauka
Kisebengo wewe Dada, utakuja kuumbuka
Acha umbea Hamida, utakuja nikumbuka
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

11. Ratiba unazijua, za kuvaa hadi kula
Acha kuwafatilia, fanya yako au zila
Utakuja kuungua, acha hiyo Silsila
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

12. Chakubimbi we ukoje, kuchunguza ya wenzio
Kumbe ndo mana Andunje, Otimbi Otimbilio
Ngoja siku wakukunje, umalize na kilio
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

13. Masingi umezoea, ndoa kuzitia doa
Wa'nkangala kutembea, kila nyumba kuzogoa
Utakudhuru umbea, mdomo watatoboa
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

14. Kavaa gauni baya, kitambaa cha kichina
Kisebengo huna haya, lakini wewe hauna
Kuwaombea mabaya, kutwa kucha unanuna
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

15. Nimefikia tamati, umenishinda tabia
'Meuzunisha umati, unajifanya kulia
Achana matashititi, sema basi 'natulia'
Tatizo sio umbea, shida kuongeza chumvi.

ABDALLAH KALINDIMA (K-mtoto)
kalindimasenior@gmail.com
NACHINGWEA

WATAKA MABADILIKO?

1. Ewe mwenye nung'uniko, usipitilize yowe
Kulaumu ya wenzako, kwakufanya uchelewe
Kutaka yende yendako, mambo udhanivyo wewe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

2. Wataka mabadiliko? Kwanza badilika wewe!
Ulitafute zinduko, chanzo chake nini kiwe
Wabadilike wenzako? Wewe ubakie jiwe!
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

3. Angalia hali yako, itathmini ijuwe
Uchunge ulimi wako, ya wengine ubeuwe
Juwa si uwezo wako, ya watu uyaongowe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

4. Kula kisogo wenzako, kila lao utongowe
Huleta mgawanyiko, udugu iubomowe
Huzalisha machafuko, umoja iutenguwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

5. Mja kamili hayuko, wajikwezaje mwenyewe
Kwenye macho ya wenzako, watafuta changarawe
Lakini hujali yako, yapofuke, yang'olewe!
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

6. Mengi madhaifu yako, iwapo yahesabiwe
Lilia madhambi yako, ujute ughufiriwe
Lishike langu andiko, sione maruweruwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

7. Una mtihani wako, na mudao upangiwe
Jibu masuali yako, ya watu usifunuwe
Utapata fadhaiko, na mwisho ulaumiwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

8. Ndugu wacha chokochoko, mbinguni ilaaniwe
Haina ila mchoko, moyo wako iuuwe
Mwisho upate anguko, vipande upasuliwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

9. Omba jema pumziko, ulifikie mwishowe
Utaulizwa ya kwako, uliyotenda mwenyewe
Haiwezi ya wenzako, uitwe uhukumiwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

10. Chunga baiati yako, kwa dhati uichukuwe
Hapo ndipo sala zako, zipae zipokelewe
Kisha ulipwe ridhiko, la Mola urehemewe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

11. Kukumbushana kumbuko, lazima kushikiliwe
Isije mkanganyiko, visivyo ninukuliwe
Lakini pia ni mwiko, dhana mbaya zidhaniwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

12. Ukileta badiliko, baraka ubarikiwe
Likuzwe lako tamko, uhai lipuliziwe
Ndio siri ya mwitiko, wengine wafufuliwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

13. Neno bila badiliko, ni chukizo lichukiwe
Mbaya wake mnuko, mavumbini lifukiwe
Mola halipi mwinuko, chafu lidharauliwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

14. Wapenda mabadiliko, sote hili tutambuwe
Tushike hiki kishiko, pamoja tuokolewe
Wakungojewa hayuko, aanze afuatiwe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

15. Ewe Mola waja Wako, wanyonge Utuzinduwe
Tupambe mapambazuko, Njiayo tuangaziwe
Tufunike kifuniko, tusione nyinginewe
Kwanza badilika wewe, utakapo badiliko!

Abdulrahman M. Ame

JIUNGE KUNDI LENYE IMAM

1. Ndugu mlie simama, Enyi mlio pembeni,
Jiunge Masihi zama, Ndiye mjumbe amini,
Mje kwenye usalama, Kundi lilo na imani,
Jiunge Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

2. Ndiko kuliko salama, ya maisha duniani,
Mje mpate salama, Mbele ya wenu manani,
Kundi hilo ndilo shima, Kizingatia kanuni,
Jiunge Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

3. Suni mbona mko nyuma, Kundi kulikataani,
Msome vitabu hima, Ukweli kuubaini,
Msibaki sema sema, Kwajeuri kulilani, Jiunge
Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

4. Sibaki kulilaani, Kundi lililoimani,
Chunguzeni umakini, Ndiko kuliko nidhamu,
Utume twauthamini, Wote tunauheshimu,
Jiunge Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

5. Kejeli weka pembeni, Chunguzeni vema kwani,
Ujumbe huu makini, Msibaki nyuma kwani,
Mjiung ' humu ndani, Kuna radha ya imani,
Jiunge Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

6. Masihia waiteni, Enyi mlio pembeni,
Kwa heshima itikeni, Mwito wenye thamani,
Muitikenijamani, Atuongoze imani,
Jiunge Jumuiyani, Kundilo Imam moja.

Madumla Ng'amilo

NAWAKUMBUKA

Ingawa hatuonani, nawakumbuka Wa Mamba
Ndugu zangu wa imani, tukikutana kuomba
Ni pale msikitini, baiti Yake Muumba
Na Inshala yatakwisha, atapopenda Rabuka
Na maradhi yanatishia, twaomba kusalimika

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Busara za Iyas ibn Muawiyah

Mtu mmoja alifika kwa Iyas Ibn Mu'awiyah, Jaji Muislam maarufu kwa busara zake, na mazungumzo yafuatayo yalifanyika kati yao:

Mtu: Je ni ipi hukumu ya Islam kuhusiana na mvinyo?
Hakimu: Ni haramu (ni mwiko).



Mtu: Vipi kuhusu maji?
Jaji: Ni halali (yameruhusiwa).

Mtu: Vipi kuhusu tende na zabibu?
Jaji: Ni halali.

Mtu: Kwa nini ya kwamba hivi vitu vyote ni halali, na bado ukivichanganya vinakuwa haramu?
Jaji alimtazama yule mtu na akamwambia: Endapo nitakupiga na mchanga kiasi, unafikiri utakuumiza?

Mtu: Hautoniumiza.
Jaji: Vipi kama nitakupiga na ukufi wa mabua?

Mtu: Hayatoniumiza.

Jaji: Vipi kuhusu maji kidogo?
Mtu: Bila shaka Hayatoniumiza.

Jaji: Vipi kama nikivichanganya, na kuacha vikauke liwe tofali, na nikakupiga nalo, litakuumiza?
Mtu: Itaniumiza na hata kuniua kabisa!

Jaji: Sababu hiyo hiyo inatumika kwa swali ulilonuliza!!

. . . . . .

Iyas Ibn Muawiyah Al-Muzani alikuwa Qadhi tabi'i katika karne ya 2 AH ambaye aliishi Basra (kwa sasa Iraqi). Alifahamika kwa kuwa na akili sana ambayo ilimfanya kuwa mada pendwa katika simulizi za mila za Kiarabu.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

Ada	Kheri	Shetani	Umoja	Akili
Kesi	Sheria	Umasikini	Aibu	Kudura
Shauri	Ulevi	Ahadi	Kosa	Starehe
Ukweli	Afya	Kibri	Siri	Unyamavu
Adabu	Khofu	Silika	Undugu	

N	Y	U	T	Z	K	P	S	C	L	U	D	N	M
U	L	K	F	F	T	C	R	H	B	N	N	P	U
N	S	W	U	K	U	D	U	R	A	D	Z	N	M
Y	H	E	L	M	K	H	O	F	U	U	L	V	O
A	E	L	E	K	A	I	S	B	M	G	R	V	J
M	T	I	V	C	D	S	A	H	F	U	A	I	A
A	A	N	I	A	S	D	I	J	E	D	K	W	C
V	N	L	H	I	A	T	V	K	A	R	W	R	Z
U	I	A	L	R	H	S	A	S	I	M	I	L	T
W	F	I	U	K	C	Y	I	R	I	N	R	A	B
N	K	B	M	B	F	T	N	R	E	L	I	K	N
A	I	K	Y	A	K	H	E	R	I	H	I	F	G
A	L	M	K	O	S	A	T	B	B	F	E	K	G
T	K	I	B	R	I	K	E	S	I	D	W	Y	A

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jifunze Kuchoma Mishikaki ya Kuku

Na **Mtandao**



Mahitaji:-

» Vidari vya kuku 2, bila ngozi wala mifupa (safisha na katakata vipande vidogo dogo)
» Mafuta 1/4 kikombe
» Chumvi na pilipili manga kiasi
» Kitunguu saumu kilichopondwa kijiko 1 1/2 cha chai
» Tangawizi ilosagwa 1/2 kijiko cha chai
» Maji ya limao 1 dogo au 1/2 kubwa
» Majani ya kotmiri yalokatwa katwa kiasi

Namna ya Kutayarisha:

1. Tia kuku wako pamoja na viungo vyote katika bakuli na changanya vizuri kwa mikono viungo vienee.

2. Funika vizuri na wacha viingie viungo kwa muda wa saa moja unaweza pia kuacha usiku kucha katika fridge kwa ladha zaidi

3. Ukitumia vijiti vya mti basi hakikisha unaviloweka katika maji baridi kwa muda wa nusu saa ili visiungue wakati wa kuchoma

4. Tunga mishikaki yako kwa idadi upendayo na kisha choma au oka hadi ipate kuiva vizuri pande zote mbili.

5. Mishikaki tayari kwa kula kwa sauce upendayo, ukitaka viungo zaidi unaweza tia manjano, binzari nyembamba ya unga na giligilani ya unga au uoendavyo. Furahia!

(kwa oveni moto uwe nyuzi joto 200)

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{AS}

Kuwarehemu Ndugu

Ninyi hamuwezi kukubalika kwake hadi dhahiri yenu na batini yenu ziwe namna moja. Warehemuni wadogo juu ya kwamba m wakubwa, wala msiwahakirishe, mkiwa wenye Elimu, wapeni nasaha walio wajinga, wala msiwadhalilishe kwa kujivuna. Na mkiwa matajiri, wahudumieni walio masikini, sio kuwafanyia Kiburi kwa kujipenda. Ziogopeni njia za Maangamio. Dumuni kumuogopa Mwenyezi Mungu na mshikamane na Ucha Mungu, ...Ni mwenye bahati mbaya alioje Mtu yule asiyeyaamini Maneno haya yaliyotoka kinywani mwa Mwenyezi Mungu ambayo nimeyabainisha. Ikiwa mwataka Mwenyezi Mungu Awe radhi nanyi mbinguni, basi kuweni wamoja kama ndugu wawili waliotoka tumbo moja. Miongoni mwenu aliye mcha Mungu zaidi ni yule anayeyasamehe zaidi madhambi ya nduguye na mwenye bahati mbaya ni yule afanyaye ushupavu, asiyesamehe.

(Safina ya Nuhu, Ruhani Khazain Jal. 19, uk 12-13)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Namna ya Kufanya Toba na Kuomba Maghofira kwa Allah

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

Na ya kwamba mwombe msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie Kwake. Atawafaidisheni kwa vifao vizuri mpaka muda maalum, na Atampa kila mwenye fadhili, fadhili yake. Na kama mtageuka, basi nawahofieni adhabu ya siku kubwa. (Surah 11:4)

Toba ni kufanya bidiii kuondoa matokeo mabaya ya dhambi na kuyavunja matamanio mabaya. Kwa hakika toba ni tendo la kuelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo wote baada ya kumwomba Akulinde na matokeo mabaya ya dhambi zilizopita.

Masih Aliyeahidiwa^{as} anasema toba ni kutumia vipawa vya mwili kuachana dhambi. Anasema mwanadamu ameumbwa na vipawa mbalimbali ikiwa na uwezo wa kuachana na dhambi. Akasema kuna hatua tatu za kufanya toba:

1. Kuepuka mawazo mabaya na matamanio mabaya. Njia hii ni ya kuchukia mawazo hayo, kuwa unapopata matamanio mabaya au mawazo mabaya mfano umemtamani mwanamamke basi mchukie. Masufi walitumia njia hii kwa kufananisha mawazo mabaya na matamanio mabaya kwa kulinganisha na sokwe au nguruwe wao ndio walikuwa wanawachukia hao wanyama. Ila wewe chagua kitu chochote ambacho hukichukia basi linganisha mawazo hayo mabaya na jambo hilo ambalo hulichukia. Hapa Allah Ameumba chuki ili kuchukia uovu ila sio kitu kingine sisi tumebadili kwa kuchukia wema na mema.

2. Kujutia matendo mabaya uliyofanya. Ukiwa umefanikiwa kufanya uovu wowote na ukatambua umefanya uovu. Jijengee uwezo wa kujilaumu na kujutia uovu huo, hali hii itakuja kwa kutambua na kujielimisha wema wake. Tafuta wema wa tendo ulilofanya uovu ili majuto yazalikane. Tambua uovu ni uasi wa wema.

3. Jidhatiti kutorudia makosa au maovu. Ni kupita katika njia ambazo zilikutelezesha na kuziepuka hapa. Kama hijjab madhalani jitahidi uvae, uinamishe macho, usichanganikane hovyo wanaume na wanawake, kujikita katika ibada zote na njia za kujitolea n.k

Masih Aliyeahidiwa^{as} anasema jitihada hizi zote ni kazi bure na haiwezekani bila kuwa na nguvu ya Allah na nguvu zote awezazo kutumia vipawa vyake mwanadamu hutegemea nguvu ya Allah 2:166. Hivyo toba yeyote haifanikiwi bila istighfar na istighfar ndio nguvu ya toba na katika aya hii 11:4 istighfar imetangulia dhidi ya toba. Hivyo wazi njia za toba zitafanikiwa ikiwa istighfar itafanyika kwa ukamilifu wake ili upate uwezo wa kuchikia dhambi, kujutia dhambi na kujidhatiti kutofanya makosa tena.

Istighfar (Kuomba Ghofira) ambalo maana yake hasa ni Kumwomba Allah Afunike. Kwa maana hii mradi wake itakuwa ya kwamba tumwombe Allah siku zote Afunike maelekeo yetu ya uovu na matamanio yanayotuzuia katika kumkaribia.

Njia ya istighfar imefunzwa ndani ya Quran Tukufu na Hadith za Mtume^{saw} na namna mbalimbali za toba sawa na makosa zimefunzwa. Makatazo yote na mafundisho yote ya namna ya kuishi hapa duniani ni njia zote zenye kukuhakikishia toba yenye ukamilifu. Kama zinaa angalia namna ya kusikiliza sauti ya wanawake, kuangalia, hijab, dansi, n.k angalia makatazo ya kusema, kusikia, sauti, pombe, kamali, chakula n.k

Allah Atujaalie kufanya istighfar na toba zilizokamilika. Amin

Ukweli wa Tamaa na Jinsi ya Kuziepuka.

Tamaa na matumaini kuhusu suala fulani ni silika ya asili ya mwanadamu, tunachofundishwa na dini yetu au dini zote ni kwamba tuweze kuziendesha hizi tamaa zetu kuelekea mlengo wa kulia na sio hizo kutuendesha sisi.

Kuna jinsi ya kuziepuka hizo tamaa mbaya na baadhi ya Wacha Mungu waliopita wanaeleza kuwa:

Ukiona vyenye kutamanisha vione kama umeona mtu ambaye yupo msalani na anajikidhi haja zao, hivyo utageuka kwa kuepuka kuona tupu zake na utaziba pua kwa kuepuka harufu mbaya ya haja na utaenda mbali na eneo hilo, hivyo ndivyo fanyeni kwa kuziepuka tamaa mbaya za maisha ya dunia na tamaa zake.

Na akasema; Maisha ya dunia na ladha zake ni sumu ambayo kwa nje inaonekana laini na yenye kuvutia ila kwa ndani jeraha lake ni kali na lenye kuangamiza.

Sayyidna Ahmad^{as} alisema: *Tamaa ni kama dutu la ukurutu au kipele jinsi kiwashavyo, na pindi unapokitii na kukikuna ndivyo utamu unavyoongezeka ila kadiri unavyozidi kukuna mwishowe huvimba na huwa donda lenye athari kubwa. Ila kama ukiacha na kupuuzia muwasho wake mwishowe hutulia chenyewe.*

Na **Sheikh Shabani Shunda**

MATUKIO KATIKA PICHA





Khuddam wa Ikwiriri, Pwani wakichangia Damu na kupata chupa 10





Mwalimu wa Tawi la Nguruka akiongea na wanakaya wakati wa ziara ya kimalezi ya nyumba kwa nyumba



Sadr MKAT pamoja na Khuddam waliochaguliwa kuendelea na elimu ya juu 2020







Wajumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya wakiwa katika kanisa la Waadventista Wasabato baada ya mwaliko wa moja ya tukio lao.



Mjadala wa amani wa kidini kati ya Sunni toka masjid Aqswa-Kahama na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, ambapo wageni walipata nafasi ya kuondoka na zawadi ya vitabu.











Wanajamaat wakiwa katika Wakal Amal ya usafishaji wa maeneo yote ya Jamaat huko Kitonga.

Safari ya Sialkot ya Seyidna Ahmad[as] 1904



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Seyidna Ahmad[as] Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliponuia kuenda Sialkot, basi tarehe 27 Oktoba 1904 saa kumi asubuhi Hudhur[as] alitoka Qadian, ahli zake pia walikuwa pamoja. Kutoka Batala stesheni behewa moja ya daraja ya pili na behewa moja ya wastan zilipangwa. Wakati wa kufika Amritsar wanajumuiya wa pale waliwaletea chakula, Hudhur[as] alichokubali. Garimoshi lilipofika Lahore watu walijumuika kwenye stesheni kiasi hiki kwamba ilikuwa gumu kwa maafisa wa reli na polisi kupanga. Kwenye stesheni ya Wazirabad pia watu walikuwa wengi kiasi hiki kwamba ikawa gumu kwa wafanyakazi wa reli kuondoa behewa yake iliyopangwa kwa kuunganisha na gari la Sialkot. Wanajumuiya wa Wazirabad pia waliwapatia Hudhur na wenzake soda na sharbati ya limau.

Kufika Sialkot:

Ingawa gari lilifika Sialkot stesheni baada ya magharibi, hata hivyo stesheni ilijaa sana mno kwa wenye shauku ya kumwona. Hudhur[as] kwa wenzake walipopanda magari kwa kuenda pahali pa kukaa, nje mpaka mwisho wa kuona walikuwa watu tu. Mamia ya watu walikimbia pamoja na gari lake. Agha Muhammad Bakir Khan, Hakimu wa heshima alitembea mbele ya gari la Hudhur[as] kwa kupanga watu. Njiani kwa kuweka mwanga mbele ya gari la Hudhur[as] mioto iliwashwa. Ilipangwa kukaa kwa Hudhur[as] katika nyumba ya Hadhrat Hakim Hisamuddin.

Karamu ya wanajumuiya wa Sialkot:

Kwa vile nyumba ya Hadhrat Hakim haikutosha kwa kukaa kwa ndugu wato, kwa hiyo wanajumuiya wengi wa maeneo yale waliacha nyumba zao kwa wageni kwa njia hii kwamba mitaa yote yakawa kama nyumba moja. Katika kila chumba maji na mwanga wa kutosha ulipangwa. Jumuiya ilipanga maduka ya waganga wa mji kwa kupata dawa bure. Mpango wa chakula ulikuwa hivi kwamba wageni kutoka Qadian walikuwa wakipewa chakula makazini mwao na wageni wengine waliokuja kutoka wilaya za Sialkot, Gujaranwala, Lahore, Jehlum, Gujrat na kadhalika walikuwa wakipewa chakula katika uani moja kubwa.

Ukaribisho:

Nilisahau kutaja kwamba wakati wa ujio wa Hudhur[as] katika Sialikot, Jumuiya iligawa ukaribisho uliochapwa ambamo ziliandikwa beti hazi mbili:

Ujio wako ni raha kwetu, kukutaja ni nyimbo ya furaha yetu.
Ee mola, weka kivuli chako juu ya moyo wetu mpenda, ee Khidhiri wetu, Mahdi wetu, Isa wetu na Mirza wetu.

Hotuba ya Hudhur[as] baada ya sala ya Ijuma:

Siku ya pili tarehe 28 Oktoba ilikuwa Ijuma. Sala ya Ijuma katika Msikiti wa Hadhrat Hakim Hisamuddin, Hadhrat Maulawii Abdul Karim alisalisha na katika hotuba ya Ijuma alieleza maelezo ya Sura Al-Jumu'a. Baada ya sala watu wengi walifanya baiati, Kwa vile idadi ya wafanyao baiati ilikuwa kubwa sana, kwa hiyo vilemba 12 vilisambazwa kwa jeha mbalimabli, watu wakivishika walirudia ahadi ya baiati. Baada ya baiati Hudhur[as] alitoa hotuba fupi ambamo alieleza uhakika wa baiati na alisisitiza kutanguliza dini juu ya dunia. Hotuba hiyo ilichapwa katika magazeti ya Jumuiya. Baada ya sala ya Ijuma kwa kukaa na watu kwa muda mrefu hali ya Hudhur[as] iliathirika vibaya, kwa hiyo siku mbili zijazo yaani 29 na 30 Oktoba Hudhur[as] hakuweza kuja nje. Tarehe 31 Oktoba 1904 Hudhur[as] alidhihirisha nia yake ya kurudi, kwani wageni walijumuika zaidi sana ya mategemeo na Hudhur[as] alihofia sana kwamba isije Jumuiya ya Sialkot itaabike kwa kuwalisha wageni. Hadhrat Hakim alipojua jambo hilo basi mara alimfikia Hudhur[as] na akitaja akiba ya vyakula vyake alimwomba Hudhur[as] kuahirisha nia yake. Hudhur[as] alimjaali sana Bwana Hakim kwani alikuwa na mahusiano naye tangu siku za kuajiriwa katika Sialkot. Kwa hiyo aliahirisha nia yake ya kurudi.

Pendekezo la hotuba ya hadharani:

Iliamuliwa kwamba katika Sialkot hadhara moja ipangwe. Basi kwa lengo hilo baada ya kupanga tarehe 2 Novemba 1904 ilitangazwa kwa matangazo na Hudhur[as] alishughulikia kutayarisha hotuba. Kwa hiyo tarehe 31 Oktoba 1904 pia Hudhur[as] hakuweza kuja nje. Idadi ya wapendao kumwona iliendelea kuzidi. Kuona hali hiyo Hudhur[as] aliombwa kwamba akae kwa muda fulani katika dirisha la ghorofa ili watu waweze kumwona kutoka mitaani. Hudhur[as] akaja dirishani lakini kwa kujumuika maelfu ya watu, alihofia kwamba isije mzee, mtoto au dhaifu yeyote akanyagwe na halaiki, akisimama kwa dakika moja tu alirudi.

Alikuwa na ufululizo wa kalamu kiasi hiki kwamba Baadhi ya wakati aliandika kitabu cha mamia ya kurasa katika siku chache. Hotuba ya Sialkot iliyo hotuba ya juu sana, Hudhur[as] alianza kuiandika baada ya adhuhuri ya 31 Oktoba na tarehe mosi Novemba ilichapwa tayari. Hotuba ilikuwa juu ya "Islam" iliyopangwa kusomwa katika nyumba ya wageni ya Maharaja Jammu tarehe 2 Novemba 1904 saa moja asubuhi. Mkutano ulifanyika katika uani wa nyumba ya wageni ya Maharaja Jammu ambamo ilipangwa mikeka na mahema kwa uwingi.

Kwa vile Hadhrat Maulawii Abdul Karim akija kabla ya Hudhur[as] alitoa hotuba mbili katika mji hadharani na matangazo pia yalisambazwa kwa uwingi, kwa hiyo masheikh wapinzani kwa kuzuia watu kufika mkutanoni siku hiyo asubuhi saa kumi na mbili na nusu walianza kutoa hotuba za kukataza katika sehemu mbali mbali mjini. Hata hivyo watu walijumuika kusikiliza hotuba ya Hudhur[as] wengi kiasi hiki kwamba ikawa gumu kupanga kuwakaisha.

Kuenda mkutanoni:

Hudhur[as] alienda mkutanoni kwa sura ya msafara, kwa magari 15-16. Hadhrat Maulawii Abdul Karim alikaa na Hudhur[as] na kwa gari la Hudhur[as] kwa kupanga njia Sardar Muhammad Yusuf Khan, Hakimu wa mji alikuwa akitembea. Pande zote mbili halaiki ilijumuika kwa uwingi kiasi hiki kwamba kwa taabu sana njia ilipatikana kupitia magari. Njiani majukwaa ya masheikh wapinzani pia yalionekana. Masheikh walizuia watu kuenda mkutanoni kwa kupaza sana sauti lakini matokeo yake yalikuwa haya kwamba watu waliojua tayari mahali pa Mkutano walielekea huko lakini ambao hawakujua pia kwa hotuba za masheikh walipajua na walienda mbio mkutanoni. Mungu Akitaka adui pia anasababisha heri.

Hotuba ya uraisi ya Hadhrat Maulana Nuruddin[ra]:

Hudhur[as] alipofika mkutanoni, aliona kwamba maelfu ya watu wa kila dini na kabila wameshajumuika. Waheshimiwa wa mji walikuwa na rai hii kwamba mpaka leo katika Sialkot watu wengi kiasi hiki hawajaonekana katika hotuba ya mtu yeyote. Kwenye jukwaa pamoja na Hudhur[as] walikaa Hadhrat Maulawii Abdul Karim na wazee wengine. Baadhi ya waheshimiwa wa mji pia walikaa hapo. Kwa maoni ya Mian Fadhl Husain Barrister na kwa kuungwa mkono na wahudhuriao Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin akawa mwenyekiti wa mkutano. Katika hotuba yake nzuri na fupi aliwaambia wahudhuriao kwamba watu ambao kutosikiliza mambo yao watu watalazimika kusema siku ya kiyama kwamba:

لو كنا نسمع او نعقل ما كنا فى اصحاب السعير

Laiti tulikuwa tunasikia na kutafakari kwa kutumia akili basi leo tusingepata taabu. mfano wa watu hao mtasikiliza hotuba yake saa hii. Kwa hiyo sikilizeni kwa makini na mmifuate.

Hotuba ya Hudhur[as]:

Baada yake alimwomba Hadhrat Maulawii Abdul Karim kusoma hotuba ya Hudhur[as] Hadhrat Maulawii Abdul Karim mwanzoni alisoma kwa sauti nzuri na kubwa fungu la mwisho la Sura Al-Hashr kisha alianza kusoma hotuba ya Hudhur[as] kwa njia safi sana ya kuvutia. Kueleza mandhari ya wakati ule ni nje ya uwezo wetu. Watu kwa makini sana walisikiliza hotuba ya Hudhur[as] hata watu wengi walisimama juani pia.

Sifa kubwa ya hotuba hiyo ilikuwa hii kwamba akieleza madai yake mara ya kwanza kabisa alijitaja kama mithili wa Karishna pia. Kisha akiwahutubia Mabaniani na Maariya alisema kwamba nawasihini hivi kwa kuwa Karishna kwamba kuamini ya kuwa mata na roho ni tangu azali na za kudumu pamoja na Mwenyezi Mungu ni itikadi batili na iliyojaa na ushirikina. Kwa hiyo iacheni itikadi hiyo. Vile vile alisema kwamba itikadi ya tanasukh pia ni batili na Niyoga ni kitendo kichafu kiasi hiki kwamba ni aibu kuieleza pia. Baada ya hotuba kumalizika wakati wa kurudi makazini kwa wenzake katika gari lililofungwa, njiani wapinzani walianza kupiga mawe garini lakini kwa fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu Hudhur[as] alifika makazini kwa usalama. Kwa kuona fitina za wapinzani, Inspekta polisi Mzungu wakati ule aliyekuwa kazini, aliwaambia masheikh; "twashangaa kwamba kwa nini mnampinga mtu huyu, twapaswa sisi Wakristo au Mabaniani kumpinga kwani anapinga dini yetu. Anathibitisha Islam kuwa dini ya kweli, anaangamiza dini yetu, mnampinga bure."

Uwingi wa wafanyao baiati:

Tarehe 3 Novemba 1904 ilipangwa kwa kurudi kwa Hudhura.s., Kwa hiyo tarehe 2 Novemba yaani siku ya hotuba watu wengi walif siku ya hotuba watu wengi walifanya baiati juu ya mkono wa Hudhur as.

Baiati ya Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan:

Mheshimiwa Chaudhari Asdullah Khan Barrister, Amiri wa Jumuiya ya Waahmadiyya ya Lahore anasema kwamba baba yetu (Chaudhari Nasrullah Khan) pia alifanya baiati tarehe 2 au 3 Novemba tu na mama yetu alitangulia siku chache kufanya baiati kulingana na ndoto yake. Baba alikuwa mtu wa kutazama mambo kwa makini sana na alijua vizuri hali za Hudhur as. Katika kesi ya Sheikh Karmuddin Hudhur[as] alimwita baba pia kama shahidi. Na kabla ya ushahidi alisema kwamba Bwana Chaudhari, katika ushahidi wako useme ile tu unayojua, kwayo baba aliathirika sana. Ukweli wa Jumuiya alijua hivi kwamba katika Sialkot Cantt ulikuwepo msikiti, imamu na msimamizi wake alikuwa Hadhrat Maulawii Abu Yusuf Mubarak Ali. Kwa vile alikuwa Mwahmadiyya, kwa hiyo msikiti pia ulikuwa chini ya usimamizi wa Waahmadiyya. Baada muda fulani wasiokuwa Waahmadiyya walitaka kunyanganya msikiti huo. Hudhur[as] alipoambiwa alisema kwamba kama Chaudhari Nasrullah Khan akikubali basi mfanyeni wakili katika kesi yenu. Kwa kufuatilia kesi barambara ilikuwa lazima kwamba asome vitabu vya Hudhur as. Basi alifanya hivyo. Alipohudhuria mahakamani aliona kwamba Kwa

Endelea uk 11

Safari ya Sialkot ya Seyidna Ahmad as 1904

Kutoka uk. 10

kupinga Waahmadiyya masheikh wakubwa wakubwa wanakuja na wanasema uongo bila kusita lakini kila shahidi Mwahmadiyya anasema jambo lile tu analojua kwa yakini na kuchukia sana kusema uongo. Baba alichunguza kwa makini sana mwenendo wa Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya na aliathirika sana na ushahidi wa Waahmadiyya. Wakati fulani hakimu alipomwuliza kwamba Bwana Chaudhari, je, u pia Mwahmadiyya? Hapo baba alisema kwamba sikukuwa Mwahmadiyya lakini sasa inaonekana nitalazimika kuwa Mwahmadiyya na kwa kuithibitisha alieleza matukio ya kesi. Na kasema kwamba mtu ambaye wafuasi wake wanayo hali hii kwamba hawana cheo chochote cha dini lakini hata kuona hasara yao wazi wazi hawakosi kusema ukweli, basi mtu yule mwenye wafuasi wa aina hii hali yake itakuwaje. Nilikuwa nilisema kwamba siku ile watu wengi walifanya baiati. Baada ya baiati Hudhur as alitoa hotuba ya nasaha ambamo alieleza makusudio ya baiati.

Sialkot ulikuwa mji ule amabmo aliishi kikazi kwa miaka minne kuanzia 1864 hadi 1868. Lakini katika zama zile watu wachache tu walijuana naye na watu wengine hawakujua hata jina lake. Sasa Hudhur as alipoenda, alikuwa Mjumbe Adhimu wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kabla ya kuja kwake watu walijumuika kama vile kwa kupiga baragumu watu wanajumuishwa kwa amri. Na kwa kuona nadhara hiyo nadhara ya Jehlum ikaja mbele ya macho.

Kurudi Qadian – 3 Novemba 1904:

Tarehe 3 Novemba 1904 alitoka kwa kurudi Qadian. Nje ya makazini ya Hudhur as kama kawaida watu walianza kujumuika tangu asubuhi. Kwa kutahadhari Hudhur alituma mapema akinamama stesheni kwa Hadhrat Mir Nasir Nawab. Jamaat ya Sialkot waliwalisha wageni chakula kabla ya saa nne asubuhi. Karibu saa sita Hudhur as alishuka kutoka ghorofani. Halaiki kubwa ilijumuika. Ingawa mpango wa polisi ulikuwa imara sana hata hivyo baadhi ya wakati hao pia walishindwa. Kwa gari la Hudhur as njia ilipatikana kwa taabu sana. Hudhur as alipofika kwenye stesheni hapo pia kotekote palijaa. Kwa Hudhur as behewa moja la daraja ya pili ilipangwa. Hudhur as kwa ahli zake alipanda behewa ile. Gari lilipotoka, jukwaa ilijaa kwa sauti ya Assalamu alaikum na kwa heri.

Katika stesheni hiyo ilitokea kwamba gari lilipotoka jukwaa ndipo baadhi ya wapinzani wakawa uchi kwenye stesheni lakini hatuoni hapa umuhimu wake kueleza. Lakini kitendo hicho kilikuwa kinyume cha Islam bali kinyume cha ubinadamu kiasi hiki kwamba hata gazeti pingaji kali la Jumuiya Ahmadiyya "Ahle Hadithi" pia lililazimika kulalamika.

Stesheni ya Wazirabad:

Gari lilipofika Wazirabad, kwenye jukwaa la garimoshi hapo msongamano ulikuwa kubwa zaidi kuliko awali. Hadhrat Hafidh Maulawii Ghulam Rasul Wazirabadi, kama awali, aliwahudumia ndugu zake kwa sharbati ya limau na soda. Mungu Ampatie ujira bora.

Kwenye stesheni ya Wazirabad garini pia watu wengi walifanya baiati. Wakati wa kurudi katika Lahore Daktari Seyid Muhammad Husain Shah aliwahudumia Hudhur as na wenzake kwa chakula cha jioni. Usiku Hudhur as alikaa Batala, asubuhi Jumuiya ya Batala ilileta chai na chakula. Hatimae karibu saa sita mchana, Hudhur as kwa ahli na mahadimu zake alifika Qadian. Alhamdulillahi alaa dhalika.

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Kutoka uk.12

Khalifa mtukufu atba anasema; Zaid bin Amr alikuwepo katika zama za Mtume saw lakini akafariki kabla ya Utume wa Mtume saw alikuwa anasema mimi ninamngoja Nabii kutoka katika ukoo wa Nabii Ismail, lakini inaonekana mimi sitaweza kuwa katika zama zake. Ewe Amir kama utakuwepo katika zama za Nabii yule basi mfikishie salamu zangu. Amir anasema mimi nikafikisha salamu za Zaid bin Amr kwa Mtume saw Mtume saw akapokea salamu yake na kumuombea dua ya rehema. Anasema mimi nimemuona akiwa peponi.

Hazrat Asmaa bint Abu Bakr ra anasema; Zaid alikuwa anasema akiwa ameegemea Ka'aba kwa mgongo wake:- Enyi watu wa kabila la Quraish hakuna yeyote miongoni mwenu aliye katika dini ya Ibrahim isipokuwa mimi. Yeye alikuwa haziki mabinti hai. Bali kama kulikuwa na mtu yeyote aliyetaka kumuua binti yake alimuambia amlete kwake atampatia matumizi. Binti alipokuwa amekuwa alikuwa anasema kama una nia ya kumchukua mchukue na kama utapendelea basi gharama ya ndoa yake nitatoa mimi. Naye alikuwa anasema Ee Mola wangu laiti kama ningejua njia bora ya kufanya ibada yako lakini mimi sifahamu vizuri. Kisha alikuwa anasujudu juu ya kiganja chake. Yeye alifariki miaka mitano kabla ya Utume wa Mtume saw

Mazungumzo haya yalihusu baba wa Hazrat Said bin Zaid ambaye alikuwa anaitwa Zaid bin Amr. Sasa hivi nitaendelea kumzungumzia Hazrat Said bin Zaid.

Safari moja Hazrat Said bin Zaid na Hazrat Umar ra walifika kwa Mtume saw na wakauliza kuhusu Zaid bin Amr. Mtume saw akajibu Mwenyezi Mungu Amsamehe Zaid bin Amr, alifariki akiwa katika dini ya Ibrahim as hivyo kila alipokuwa anamtaja alikuwa anamuombea rehema.

Khalifa mtukufu anasema: Hazrat Said bin Zaid na mkewe Hazrat Fatuma waliingia katika dini ya Islam katika siku zake za mwanzo kabla ya tukio la Darul Arqam. Ni hazrat Fatuma ra aliyekuwa sababu ya Hazrat Umar kuingia katika dini ya Islam. Khalifa mtukufu atba akarudia kusimulia kisa kile cha Hazrat Umar ra kwenda kwa dada yake na kusikia Quran ikisomwa na Mwenyezi Mungu Akamjaalia fursa ya kujiunga na Islam.

Hazrat Said bin Zaid alikuwa ni miongoni mwa waliohama mwanzoni. Yeye hakuweza kushiriki katika vita vya Badr, lakini hata hivyo anahesabiwa miongoni mwa maswahaba wa Badr. Sababu ya kutokushiriki, inasemwa kuwa Mtume saw alimtuma yeye na Hazrat Talha ra siku kabla ya vita vya Badr kwenda kufanya uchunguzi wa msafara wa Maquraish uliokuwa unatoka Syria. Wao waliendelea kukaa pale mpaka msafara ulipopita. Hata hivyo kabla wao hawajarudi Mtume saw alipata habari kuwa msafara ule ulikuwa unakuja, kwa hiyo aliwaita maswahaba na akaweka nia ya kukabiliana na msafara ule. Na kwa hiyo hawa wawili ndiyo maana hawakuweza kushiriki katika vita vya Badr. Hata hivyo wao walipata hisa ya mali ya mateka ya vita ile.

Khalifa mtukufu atba anasema: Hazrat Said ra alikuwa miongoni mwa maswahaba kumi wateule walioahidiwa pepo kwa kinywa kitakatifu cha Mtume saw Kuna simulizi moja inayosema kuwa kwenye kidole cha Hazrat Said bi Zaid kulikuwa na pete iliyoandikwa maneno ya Quran.

Yeye katika zama za Ukhalifa wa Hazrat Umar ra aliongoza jeshi wakati wa kuteka mji wa Damascus na katika vita vya Yarmuk. Alipopewa nafasi ya kuwa Gavana wa mji wa Damascus, akamuandikia Hazrat Abu Ubaida ra kuwa yeye hataki kuwa Gavana kwa sababu atakosa nafasi ya kwenda kwenye vita vya Jihad. Hivyo, Hazrat Abu Ubaida akamteua na kumtuma Yazid bin Abu Sufyan.

Hazrat Said bin Zaid ra alikuwa na tabia kwamba ushauri wowote aliokuwa anaufikiria alikuwa anausema kwa uhuru. Wakati hazrat Uthman ra alipouawa na kupata ushahidi, alikuwa anasema katika msikiti wa mji wa Kufa kuwa kile kitendo mlichokifanya kwa Hazrat Uthman ra kama mlima wa Uhud utatikisika si jambo lisilowezekana.

Hazrat Said bin Zaid ra alikuwa ni mtu ambaye dua zake zilikuwa zinakubaliwa sana. Safari moja mwanamke mmoja akamtuhumu kupora kipande cha ardhi, na shauri lake likapelekwa kwa hakimu aliyeteuliwa na Hazrat Muawiya ra Hazrat Said akamuuliza: Je, unaonaje mimi ninaweza kufanya dhuluma. Kisha akaomba dua kuwa Ee Mola wangu kama tuhuma hii ni ya uongo basi mwanamke huyu apate adhabu tayari akiwa kipofu. Ndipo alipokuwa kipofu badaae na kutumbukia katika kisima na kufa.

Yeye alifariki katika mwaka wa 50 au 51 Hijria akiwa na umri wa miaka 70 au 71. Hazrat Saad bin Waqas ra akaosha maiti yake na Hazrat Abdullah bin Umar ra akaongoza sala ya jeneza lake na akazikwa Madina. Yeye alioa mara kumi katika nyakati mbalimbali, kwake wamezaliwa watoto wa kiume 13 na wa kike 19.

Khalifa mtukufu anasema: Swahaba mwingine nitakayemgusia ni Hazrat Abdul Rehman bin Auf ra Kabla ya kukubali Islam jina lake lilikuwa Abde Amr. Yeye alikuwa na rangi nyeusi, mwenye macho mazuri, mwenye kope ndefu na mwenye pua ndefu iliyonyooka. Alikuwa na shingo ndefu, viganja vyenye nguvu na vidole vinene. Katika vita vya Uhud alijeruhiwa na baadae akawa anatembea kwa kuchechemea. Yeye alikuwa ni miongoni mwa maswahaba kumi wateule walioahidiwa pepo. Yeye alizaliwa miaka kumi baada ye tukio la jeshi la Fiil (Tembo). Yeye alikuwa ni miongoni mwa wale wachache waliokuwa hawanywi pombe wakati wa ujahili. Yeye ni miongoni mwa watu wanane wa kwanza kukubali Islam. Yeye alishiriki katika uhamiaji wote wa mara mbili wa Uhabeshi. Yeye r.a anasema tulipohamia Madina Mtume saw aliweka udugu baina yangu na Hazrat Saad bin Rabii ra. Saad bin Rabii ra akasema mimi katika maswahaba Maanswar ni tajiri zaidi, mimi nakupa nusu ya mali yangu. Mimi nina wake wawili. Nitampa talaka mmoja umuoe baada ya eda yake. Baada ya kusikia hayo akajibu Mwenyezi Mungu atie baraka katika ahli zako na mali zako. Niambie njia ya kuelekea sokoni. Basi akamuambia njia ya kwenda soko la 'Kainekaa' akaenda na kuanza kufanya biashara pale. Baada ya muda ikaonekana alama ya miski juu ya nguo zake. Mtume saw akamuuliza Je, Umeshaoa? Akajibu, Naam. Mtume saw akamuuliza; mahari ni kiasi gani? Akajibu, dhahabu yenye ujazo sawa na kokwa ya tende. Mtume saw akamuambia fanya walima hata kama ni wa mbuzi mmoja.

Yeye alipata baraka nyingi katika biashara yake kiasi hiki kwamba anasema mimi niliona hali yangu ile ambapo nilikuwa natumaini kama nikiinua jiwe popote ninaweza kupata dhahabu au fedha. Alishiriki katika vita vyote. Kuna tukio moja katika vita vya Badr ambapo kulia na kushoto kwa Hazrat Abdul Rehman bin Auf walikuwepo watoto wawili maanswar waliomuua Abu Jahl. Hazrat Musleh Maud ra ametaja kisa hiki akiwa anazungumzia kujitolea kwa watoto katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa moyo na jazba.

Khalifa mtukufu anasema: Sehemu iliyobaki itaendelea katika hotuba ijayo.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Ramad. - Shaw. 1440 AH | JUNI 2020 | IHSAN 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Muhsin ni mtu anayefanya tendo jema kana kwamba anamwona Mungu; au kwa akali ajue kuwa Mungu Anamwona (***Bukhari Kitaabul-Iiman***)

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 12/06/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema;

Miongoni mwa maswahaba nitakaowazungumzia leo mmoja wapo ni Hazrat Said bin Zaid^{ra} Baba yake anaitwa Zaid bin Amr na mama yake anaitwa Fatuma. Yeye alitokana na kabila la Adi bin Ka'ab bin Lui. Lakabu yake ni Abu Aazar na Abu Swaut pia imebainika. Yeye alikuwa na kimo kirefu, rangi ya ngano na nywele zilizojaa. Huyu alikuwa ni binamu wa Hazrat Umar^{ra} Dada yake anayeitwa Aatika aliolewa na Hazrat Umar^{ra} na dada ya Hazrat Umar^{ra} Bi Fatuma aliolewa na yeye Hazrat Said bin Zaid. Dada huyu ndiye sababu ya Hazrat Umar^{ra} kuingia katika Uislam. Baba yake Hazrat Said katika zama za ujahili pia alikuwa anamuabudu Mungu Mmoja naye alikuwa anaitafuta dini ya Nabii Ibrahim^{as} Alikuwa anasema Yule Mungu wa Ibrahim Ndiye Mungu wangu, na dini ya Nabii Ibrahim^{as} ndiyo dini yangu.

Khalifa Mtukufu^{atba} anasema; Baadhi ya watoto wanauliza:



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Je, ni kweli watu waliokuwa wanamuabudu Mungu Mmoja katika zama zile walikuwepo? Naam walikuwepo. Na Mtume^{saw} alikuwa amewazidi wote katika kufanya ibada ya Mungu Mmoja. Zaid bin Amr alikuwa ametakasika na makosa ya aina mbalimbali. Yeye aliwahi kuonana na Mtume^{saw} siku za nyuma kabla yeye hajawa Mtume. Maelezo yake yanapatikana katika kitabu cha Bukhari kama ifuatavyo:-

Inasimuliwa kwamba Mtume^{saw} alionana na Zaid bin Amr katika sehemu inayoitwa Bulda; hili ni bonde linalopatikana upande wa magharibi ya mji wa Makka. Chakula kiliwekwa mbele ya Mtume^{saw} naye akakikataa, na Zaid naye akakikataa huku akisema mimi siwezi kula nyama iliyochinjwa kwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Sawa na simulizi moja Zaid bin Amr alikuwa anaihesabu dhabihu ya Maquraish kuwa ni kitu cha aibu. Alikuwa anasema mbuzi pia ameumbwa na Mwenyezi Mungu, tena ninyi mnamchinja kwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Zaid bin Amr alipokerwa na ukafiri akaamua kufanya safari ili kutafuta haki. Inasimuliwa na Hazrat Ibn Umar^{ra} kwamba Zaid bin Amr alikwenda Syria kutafuta dini, akakutana na msomi mmoja wa Kiyahudi. Alimuuliza kuhusu dini yake ili naye aweze kujiunga nayo, lakini yule msomi alimkatalia naye akasema dini yetu imekwishaharibika. Zaid akamuuliza kinyume na hii unashauri mimi nijiunge na dini gani? Msomi yule wa kiyahudi akajibu mwanadamu anatakiwa awe HANIF. Zaid akamuuliza HANIF maana yake ni nini? Yeye akajibu dini ya Nabii Ibrahim as. Ibrahim as hakuwa myahudi wala mkristo.

Zaidi alikutana na msomi mkristo, naye pia alimuambia usiungane nasi waila utashiriki katika kupata laana ya Mwenyezi Mungu. Msomi huyu pia alimshauri kujiunga na dini ya Nabii Ibrahim as. Basi Zaid alipopata ushauri mwingi kuhusu Nabii Ibrahim as, akasema Ee Mola wangu mimi nakiri kuwemo katika dini ya Ibrahim as.

Endelea uk 11

KITABU KIPYA



Kumbukumbu Langu

Kitabu hiki kidogo lakini kilichosheheni mvuto kinalenga kuwasilisha kwa wasomaji kumbukumbu kubwa na yenye kufurahisha za mwana mweledi, Hadhrat Mirza Mubarak Ahmad, alizokuwa nazo za baba yake adhimu, Hadhrat Mirza Bashirud-Din Mahmood Ahmad, Khalifa wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi.

Pindi anapokianza kitabu, msomaji ghafla anastaajabishwa na urahisi na wepesi wa mtindo ambao mwandishi wa maana amejitahidi kuandika kumbukumbu hizi pendwa za mtu ambaye aliiongoza Jumuiya yake si tu kiimani na kiroho bali pia katika masuala ya kidunia.

Kwa ufupi na kwenye nukta, kitabu kinatoa utambuzi usio kifani katika mtindo safi na asilia wa maisha ambao Hadhrat Mirza Bashirud-Din Mahmood Ahmad alitaka kukuzia watoto wake, ili kuwawezesha kumtumikia Mungu na ubinadamu katika namna bora ambayo ni ngumu kuiwazia.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba Tsh 3,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com